

# Watoto wagonjwa wanapaswa kukaa nyumbani lini bila kwenda shule ya msingi au kituo cha malezi?




## 1. Mtoto wako amepata homa, kikohozi, kuvimba koo au kamasi puani katika saa 24 zilizopita?



- Hakikisha mtoto wako anasalia nyumbani.
- Mtoto anapaswa kupimwa COVID-19.

Ikiwa mtoto ana kamasi puani tu na anahisi vizuri, anaweza kwenda shuleni au kituo cha malezi wala hahitaji kupimwa COVID-19. Hatua hii inapaswa kuchukuliwa pia ikiwa mtoto ana mzio unaojulikana.




### Wasiliana na daktari ikiwa mtoto ana homa na:

- Mtoto hataki kucheza au kushughulika kwa vyovyote.
- Mtoto ana homa, maumivu ya misuli, amepoteza hamu ya kula, ana uzembe, kichefuchefu au kizunguzungu.
- Mtoto anashindwa kupumua na/au anapumua haraka kuliko kiwango cha kawaida katika hali ya kupumzika.

Kwa sababu watoto wachanga hawawezi kueleza wanavyohisi, huenda watanuna, kumkwambia mtu au kukasirika haraka. Ikiwa una wasiwasi kuhusu mtoto wako mgonjwa unapaswa kuwasiliana na daktari wako au huduma ya matibabu ya baada ya saa za kazi.

## 2. Kipimo hiki kinathibitisha uwepo wa COVID-19?



**NDIYO**

Mtoto wako shart asalie nyumbani. Manispaa itakuambia sheria ambazo wewe na familia yako mnapaswa kufuata wakati mtoto wako anaugua.



**HAPANA**

Mtoto wako anaweza kwenda shuleni au kwenye kituo cha malezi akipata nafuu zaidi na akipona homa. Mtoto anaweza kwenda shuleni au kwenye kituo cha malezi hata ikiwa bado ana dalili ndogo kama vile kamasi, sauti yenye mkwaruzo kidogo au kikohozi kidogo.